

END OF TERM 1 EXAMS

KISWAHILI

FORM FOUR

KISWAHILI KARATASI YA 3 - FASIHI

TIME 2hrs 30 mins

NAME.....ADM NO:.....

SIGN.....INDEX NO:.....

Swali la lazima.

1. **Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu. Wanyama hawa waliishi baharini. Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba. Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika. Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko, matikitimaji na kadhalika.

Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa. Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza. Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka.

Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

Maswali

- (a) Tambua utanzu na kijipera chake. (al.2)
- (b) Taja fomyula zingine mbili za kutanguliza kifungu hiki. (al.2)
- (c) Eleza umuhimu wa kijipera hiki. (al.5)
- (d) Eleza sifa za kifungu hiki. (al.5)
- (e) Eleza umuhimu wa fomyula:
 - (i) Kutanguliza (al.3)
 - (ii) Kuhitimisha (al.3)

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657

TAMTHILIA ; KIGOGO NA TIMOTHY AREGE

2. Tulipoanza safari hii matangazo yalikuwa bayana, dhahiri shahiri babu!
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
(b) Tambua mbinu za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki. (al.4)
(c) Eleza matatizo yanayoikumba safari inayorejelewa. (al.12)
3. Eleza nafasi ya mwanamke katika jamii ya kigogo. (al.20)

RIWAYA YA CHOZI LA HERI NA ASHUMTA K. MATEI

4. Matatizo mengi yanayowakumba wahusika wengi katika riwaya hii ni mwiba wa kujidunga. Jadili (al.20)
5. Kwa kurejelea riwaya hii, fafania mbinu zifuatazo. (al.20)
- (i) Kinaya
(ii) Mbinu rejeshi
(iii) Sadfa
(iv) Jazanda

HADITHI FUPI : TUMBO LISILISHIBA.

6. Kwa kurejelea hadithi ya *Mapenzi ya kifaurongo* na *shogake dada ana ndevu* fafania changamoto zinazowakumba vijana. (al.20)
7. ***Mame Bakari***
“Una nini ? Umeshtuka mwanangu ! Unaogopa? Unaogopa nini?”
(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)
(b) Tambua mbinu **mbili** za lugha zilizotumika katika dondoo. (al.2)
(c) Eleza sifa za mrejelewa. (al.6)
(d) Eleza umuhimu wa msemaji. (al.4)
(e) Tambua maudhui yanayojitokeza katika kifungu hiki. (al.1)
(f) Fafania maudhui katika swali la (e) kwa kurejelea hadithi nzima. (al.3)

USHAIRI.

Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

Sinusubuwe akili, nakusihi e mwandani
Afiya yangu dhahili, mno nataka amani
Nawe umenikabili, nenende sipitalini Sisi
tokea azali, twende zetu mizimuni Nifwateni sipitali, na
dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini
Kwa nguvu ya kirijali, mkuyati uamini Kaafuri
pia kali, dawa ya ndwele fulani Nifwateni sipitali, na
dawa ziko nyumbani.

Mtu akiwa halali, tumbo lina walakini
Dawa yake ni subili, au zogo huauni
Zabadi pia sahali, kwa maradhi yalo ndani Au
kwenda wasaili, wenyewe walo pangani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mtu kwenda sipitali, nikutojuwa yakini.
Daktari kona mwili, tanena kansa tumboni
Visu vitiwe makali, tayari kwa pirisheni Ukatwe kama
figili, tumbo nyangwe na maini
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Japo maradhi dhahili, kuteguliwa tegoni,
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani
Waambiwa damu, kalili ndugu msaidieni
Watu wakitamali, kumbe ndio buriani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mizimu wakupa kweli, wakueleze undani
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu dhamani
Ulete kuku wawili, wamajano na wa kijani Matunda
pia asali, vitu vyae chanoni Nifwateni sipitali, na
dawa zi mlangoni?

Maswali.

1. Lipe shairi hii anwani mwafaka. (al.1)
2. Toa sababu zinazofanya mshairi kutaka kwenda hospitali. (al.3)
3. Andika ubeti wanne kwa lugha ya nathari/ tutumbi. (al.4)

FOR MARKING SCHEMES CALL/WHATSAPP 0705525657

4. Taja bahari **mbili** zilizotumika katika shairi hili. (al.2)
5. Tambua nafsini katika shairi hili. (al.1)
6. Tambua toni ya shairi hili. (al.1)
7. Eleza muundo wa shairi hili. (al.4)
8. Fafanua uhuru wa mshairi unavyojitokeza katika shairi hili. (al.2)
9. Andika maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hili. (al.2)
 - (i) dhalili
 - (ii) azali